



JAMHURI YA MUUNGANO WA  
TANZANIA  
-----  
TUME YA HAKI ZA BINADAMU  
NA UTAWALA BORA



Februari 2, 2024

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### THBUB kufuatilia haki za wafanyakazi katika makampuni ya ulinzi

**Kuanzia Februari 5 – 10, 2024 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inatarajia kufanya ufuatiliaji kuhusu utekelezaji wa haki za wafanyakazi na viwango vya ajira sehemu za kazi.**

Utuatiliaji huo unatarajiwa kufanyika katika mikoa ya Iringa, Dar es Salaam na Kagera na utahusisha kampuni binafsi za ulinzi.

Kazi hii inalenga kufuatilia utekelezaji wa Sheria na Kanuni zinazoyataka makampuni ya aina zote kutekeleza majukumu yao kwa kuheshimu haki za binadamu na upatikanaji wa suluhisho na fidia kwa wahanga wa ukiukwaji wa haki za binadamu unaohusishwa na shughuli za kibiashara au uwekezaji.

Hivyo, miongoni mwa maeneo yatakayoangaliwa katika ufuatiliaji huo ni pamoja na: Mikataba ya ajira, iwapo inakidhi viwango vya ajira; afya na usalama kazini; na utunzaji wa taarifa binafsi za waajiriwa.

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

Ploti Na. 339, Mtaa wa Nyerere – Kilimani, S.L.P 1049, DODOMA/ Ploti Na. 201, Mtaa wa Mweni, S.L.P 285, ZANZIBAR

Simu: +255 734 047 775/734 119 978 (Makao Makuu); +255 (24) 2230494 (Zanzibar)

Barua Pepe: [info@chragg.go.tz](mailto:info@chragg.go.tz), [zanzibar@chragg.go.tz](mailto:zanzibar@chragg.go.tz); Tovuti: [www.chragg.go.tz](http://www.chragg.go.tz)

Maeneo mengine ni: Uwepo wa vyama vya wafanyakazi; mahusiano ya kampuni za ulinzi na jamii; na stahili nyingine wanazopaswa waajiri kutoa kwa wafanyakazi wao.

Baada ya ufuatiliaji huo, Tume itatoa taarifa yenye mapendekezo ya namna ya kuboresha uzingatiaji wa haki za wafanyakazi na viwango vya ajira katika makampuni binafsi ya ulinzi.

Utekelezaji wa kazi hii ni mwendelezo wa ufuatiliaji wa masuala ya biashara na haki za binadamu nchini. Kwa mfano, Mwezi Desemba 2023 Tume ilifanya tathimini ya utendaji kazi kwa taasisi zisizo za kimahakama zinazoshughulikia malalamiko na migogoro inayohusiana na masuala ya biashara na haki za binadamu.

Tume inatoa shukrani zake za dhati kwa Serikali kwa kuipatia mazingira wezeshi kutekeleza majukumu yake, na kwa Taasisi ya Haki za Binadamu nchini Denmark (Danish Institute for Human Rights - DIHR) kwa kuiwezesha kiufundi na kirasilimali kufanikisha utekelezaji wa kazi hii na nyingine zilizotangulia.

Imetolewa na:



Mathew P. M. Mwaimu (Jaji Mstaafu)

**Mwenyekiti**

## **TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

Februari 2, 2024

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

Ploti Na. 339, Mtaa wa Nyerere – Kilimani, S.L.P 1049, DODOMA/ Ploti Na. 201, Mtaa wa Mbweni, S.L.P 285, ZANZIBAR

Simu: +255 734 047 775/734 119 978 (Makao Makuu); +255 (24) 2230494 (Zanzibar)

Barua Pepe: [info@chragg.go.tz](mailto:info@chragg.go.tz), [zanzibar@chragg.go.tz](mailto:zanzibar@chragg.go.tz); Tovuti: [www.chragg.go.tz](http://www.chragg.go.tz)